Ecolebooks.com

# DARASA LA NANE (8) MUHULA WA KWANZA MWAKA 2020

KISWAHILI Muda: **Saa 1 Dakika 40 Min**

***Soma vifungu vifuatavyo. Vina nafasi 1 hadi 15. Kila nafasi umepewa majibu manne. Jaza kila pengo kwa jawabu lifaalo.***

Udanganyifu katika mitihani ya _____**1**____ _____**2**___tatizo sugu kwa baraza la mitihani nchini. Hulka hii huanza katika mitihani ya kawaida na _____**3**____ kabisa kwani __**4**___ . kichocheo kikuu cha hali hii ni ile hamu ya kushindani na wengine. Takwimu zaonyesha kuwa asilimia kubwa __5__ wanafunzi __**6**__ kushiriki uovu huu wakati fulani. __**7**___wanafunzi watatumia udanganyifu kupita mitihani yao, __**8**___ wao hutatisika. Aidha taifa litakuwa na wafanyikazi ___**9**___ ipasavyo.

Daktari ___**10**___ shule yetu ili kutushauri kuhusu manufaa ya kulinda afya. Alitueleza ___**11**_____ kuwa afya bora humwezesha mtu kufanya kazi na ______**12**____mahitaji _____**13**____. Alituambia tufanye mazoezi, tuishi katika mazingira _____**14**____ na tule lishe bora. Lishe bora hutuepushia maradhi ya ___**15**____.

| | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **1.** | **A.** | taifa | **B.** | kitaifa | **C.** | mataifa | **D.** | kimataifa |
| **2.** | **A.** | imekuwa | **B.** | umekuwa | **C.** | limekuwa | **D.** | yamekuwa |
| **3.** | **A.** | kukolea | **B.** | kukolezea | **C.** | kukolezewa | **D.** | kukolewa |
| **4.** | **A.** | nazi mbovu harabu ya nzima | **B.** | mwangata mbili moja humponyoka | **C.** | mtego bila chombo haunasi | **D.** | tabia ni kia cha mwili |
| **5.** | **A.** | wa | **B.** | na | **C.** | ya | **D.** | za |
| **6.** | **A.** | wamewahi | **B.** | mmewahi | **C.** | kumewahi | **D.** | imewahi |
| **7.** | **A.** | kwani | **B.** | ingawa | **C.** | waama | **D.** | iwapo |
| **8.** | **A.** | ulegevu | **B.** | uadilifu | **C.** | maisha | **D.** | tabia |
| **9.** | **A.** | wasiohitimu | **B.** | wasiyohitimu | **C.** | waliyohitimu | **D.** | waliohitimu |
| **10.** | **A.** | alituzuru | **B.** | alipazuru | **C.** | aliizuru | **D.** | aliwazuru |
| **11.** | **A.** | shelabela | **B.** | Dhahiri shahiri | **C.** | Bure bilashi | **D.** | Chupuchupu |
| **12.** | **A.** | auyakidhi | **B.** | kumtosheleza | **C.** | kuipata | **D.** | kujinyima |
| **13.** | **A.** | mwake | **B.** | zake | **C.** | yao | **D.** | yake |
| **14.** | **A.** | safi | **B.** | masafi | **C.** | mbora | **D.** | nzuri |
| **15.** | **A.** | pepopunda | **B.** | surua | **C.** | utapiamlo | **D.** | Upele |

***Kuanzia swali la 16 hadi 30 jibu kila swali kulingana na maagizo uliyopewa***

**16.** Tambua sentensi yenye **po** ya mahali
A. Jua lilipochomoza walianza kazi zao.
B. Utajapo nyoka shika fimbo mkononi.
C. Mtoto wake amepona kabisa.
D. Palipochomewa taka huwa na majivu.

**17.** Chagua jozi ya maneno yenye maana sawa
A. Ukuta-zaraa. B. Nafasi-fursa. C. Dosari-ndoa. D. Ari-uvivu.

**18.** Sentensi ipi ina kivumishi cha pekee? A. Maneno yenyewe yamenikata ini.
B. Maneno yale yamenikata ini.
C. Maneno machafu yamenikata ini. D. Maneno yao yamenikata ini.

DOWNLOAD MORE RESOURCES LIKE THIS ON ECOLEBOOKS.COM

**19.** **"Kilimo ni uti wa mgongo wa taifa"** Hii ni fani gani ya lugha?
A. Tashbihi B. Tanakali
C. Nahau D. Sitiari

**20.** Kamilisha nomino ambata
Komba ______
A. Maji B. jungu
C. Mwiko D. kumbi

**21.** Andika kinyume cha sentensi ifuatayo;
Buda amemwuza fahali wake.
A. shaibu amemnunua fahali wake. B. ajuza amemnunua mtamba wake. C. ajuza amemwuza mtamba wake. D. buda amemnunua mtamba wake.

**22.** Kanusha;
Seremala angeiunda meza ingenunuliwa na mteja.

DOWNLOAD MORE RESOURCES LIKE THIS ON ECOLEBOOKS.COM

Ecolebooks.com

A. Seremala angeiunda meza isingenunuliwa na mteja.
B. Seremala asingeliiunda meza isingalinunuliwa na mteja.
C. Seremala asingeiunda meza isingalinunuliwa na mteja.
D. Seremala asingeiunda meza isingenunuliwa na mteja.

**23.** _____ ni malipo ya kushikia mtoto mchanga kwa mara ya kwanza.
A. Fola. B. Arbuni.
C. Utotole. D. Riba.

**24.** **Chupa** ni chombo cha kutilia vitu vya majimaji chupa pia ni;
A. Vazi la kusitiri uchi.
B. Nguo kurefuka.
C. Kumwadhibu mtoto.
D. Fuko la uzazi mwilini.

**25.** Akisami **5/8** kwa maneno ni
A. humusi tano. B. humusi nane.
C. thumni tano. D. thumni nane.

**26.** Bainisha matumizi ya **kwa** katika sentensi ifuatayo;
Alikimbia kwa kasi akaibuka mshindi
A. kuonyesha sababu ya kutenda.
B. kuonyesha nama ya kutenda.
C. kuonyesha sehemu ya kutenda.
D. kuonyesha pamoja na.

**27.** Tegua kitendawili kifuatacho;
Wamo shereheni wanakula bila mwaliko.
A. nzi. B. wezi.
C. wageni. D. moto.

**28.** Tano ni kwa chokaa kama vile____ni kwa maji
A. kichala. B. jora.
C. funda. D. doti.

**29.** Andika kisawe cha methali ifuatayo;
Ng'ombe wa maskini hazai jike.
A. liandikwalo ndilo liwalo.
B. dau la mnyonge haliendi joshi.
C. baada ya dhiki ni faraja.
D. mnyonge kapata haki ni mwenye nguvu kupenda.

**30.** Kitensi **legea** kinatupatia sifa gani?
A. ulegevu. B. legeza.
C. kulegea. D. legevu.

***Yasome makala yafuatayo kasha ujibu maswali 31-40***

Mazoea ya kusoma vitabu ni mojawapo ya raslimali kuu za binadamu. Katika kusoma msomaji hufurahia kusoma kitabu anachokimiliki kuliko katabu cha kuazima. Waama, nguo ya kuazima haisetiri matako. Kitabu kilichoazimwa ni kama mgeni nyumbani. Kitabu hicho ni lazima kitumiwe kwa uangalifu mkubwa. Sababu za uangalifu huu ni kuzuia kitabu hicho kuharibika kwa namna yoyote. Kikiwa mikononi mwa aliyekiazima. Huwezi kukiacha mahali popote au ukakiweka kwa jinsi yoyote. Huwezi kukunja kurasa zake wala kuandika chochote katika kurasa zake. Hatimaye, ingawa hili halizingatiwi sana, lazima kitabu kilichoazimwa kirudishwe kwa mwenyewe katika wakati aliopendekeza.

Hebu sasa tuangalie hali ya matumizi ya kitabu kilicho chako. Kwanza, kitabu unachomiliki utakitunza kama mboni ya jicho lako. Hata hivyo, ni muhimu kuzingatia kwamba vitabu vinadhamiriwa kusomwa na wala si kutumiwa kama urembo. Haina maana kumiliki kitabu ambacho utahofia kuandika kurasa zake au kukiweka mezani huku kurasa zake zimefunguka na zikiangalia chini au kukunja karatasi katika ukurasa ulioufikia.

Sababu kuu ya kuandika kurasa za kitabu unapokisoma ni kukuwezesha kukumbuka kwa urahisi baadhi ya mambo ambayo yamekuvutia. Pia, maandishi haya hukusudia kufanya marejeleo kwa urahisi. Hata unapotaka kurejelea jambo fulani katika kitabu hicho baada ya miaka mingi, maandishi hayo yatakuwa kama alama ulizoziacha msituni ulipoutembelea awali.

Kila mja anayethamini kusoma hana budi kuanza kujenga maktaba yake binafsi katika ujana wake. Pamoja na kwamba atakuwa na utajiri mkubwa wa vitabu katika siku zake za halafu, atapalilia kuwa na mali anayomiliki yeye mwenyewe. Maktaba ya kibinafsi yanafaa yawe na rafu wazi ambapo unaweza kukipata kitabu chochote kwa urahisi pindi unapokihitaji.

DOWNLOAD MORE RESOURCES LIKE THIS ON ECOLEBOOKS.COM

Ecolebooks.com

Je, umevisoma vitabu hivi vyote ? Hili ni swali linaloulizwa na wengi wanapoviona maktaba ya kibinafsi yamesheheni vitabu lukuki. Si lazima uwe umevisoma vitabu vyote unavyomiliki, vitabu ni hifadhi muhimu sana ya historia. Kumbuka kwamba vitabu vingi tunavyovisoma vimeandikwa ina waandishi kutoka karibu na mbali nasi, wengine walio hai na walioiaga dunia. Tunapovisoma tunapata kutangamana nao kimawazo na kuelewa hisia zao na kuwafahamu kwa undani.

**Maswali**

DOWNLOAD MORE RESOURCES LIKE THIS ON ECOLEBOOKS.COM

**31.** Nguo ya kuazima katika kifungu imelinganishwa na;
A. kusoma kitabu unachomiliki mtu.
B. mgeni anayetembea nyumbani.
C. kitabu ulichosaidiwa mtu ukisome.
D. kitabu chenye hadithi ya kufurahisha.

**32.** Lengo la mtu kukitunza sana kitabu kisicho chake ni
A. kuzuia uharibifu unaoweza kuzua ugomvi.
B. kumfurahisha mmliki wa kitabu.
C. kupendezwa zaidi na kitabu hicho.
D. kuzingatia masharti ya mwenye kitabu.

**33.** Watu wengi hawafanikiwi
A. kusoma vitabu vya kuazima kikamilifu.
B. kurudisha vitabu vya wenyewe kwa wakati ufaao.
C. kutunza vitabu vya wengine ipasavyo.
D. kuuelewa ujumbe wa vitabu walivyoviazima.

**34. Utakitunza kama mboni ya jicho lako,** maana yake ni kuwa
A. utakithamini sana.
B. hutatamani kukisoma.
C. utaenda nacho kila mahali.
D. utakilinda kisiharibike.

**35.** Kukunja, kuacha kitabu kikiangalia chini na kuandikia kurasa zake,
A. ni uharibifu wa vitabu.
B. hufanywa maktabani pekee. C. hunuiwa kumsaidia msomaji. D. hufanyiwa vitabu vya kuazima.

**36.** Mtu huacha alama msituni,
A. ili aonyeshe kuwa alikuwa huko.
B. ili asipotee atakaporejea kwenye njia aliyofuata.
C. Ili kuepuka hatari ya kuvamiwa na wanyama.
D. Ili aepuka kurudia njia hiyo baadaye.

**37.** Tunaambiwa kwamba, kwa kawaida binadamu,
A. hupenda kuwa na mali yake binafsi.
B. hujiwekea maktaba ya kibinafsi.
C. hupenda kutumia vitu vya wengine.
D. hupenda kuwasaidia wengine kwa vyake.

**38. Rafu** kulingana na muktadha ni
A. kabati kubwa la ukutani ndani.
B. uchezaji usiozingatia kanuni.
C. kitu kisicho laini.
D. bati au ubao uliogongomewa ukutani.

**39.** Kulingana na aya ya mwisho,
A. hapana haja ya kuwa na vitabu tusivyovisoma.
B. mtu anaweza kuhifadhi vitabu hata asivyovisoma.
C. maktaba ya kibinafsi sharti yawe na vitabu lukuki.
D. mja hafai kusoma vitabu vingi kupindukia.

**40.** Vitabu ni hifadhi muhimu ya historia kwa sababu,
A. Vyote kubeba maelezo ya wakati uliopita.
B. Vingi huandikwa historia ya waandishi.
C. huandikwa na watu wa maeneo na enzi tofauti.
D. vitabu huandikwa na waandishi walioaga dunia.

***Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali 41-50***

Haikuwahi kunijia akilini kwamba jambo kama hilo lingeweza kunikumba. Lilinipata kwa kasi sana. Nilididimia katika luja. Maisha yangu ya baadaye yalielekea kuingia giza kuu wala wa kuniauni hakuwepo.

Nilikulia katika kitongoji cha tujikaze na wazazi wangu na mnuna wangu. Hatukuwa matajiri lakini hatukukosa mahitaji ya kimsingi. Wazazi wangu walinikumbusha kila mara nitie juhudi masomoni angaa maisha yangu ya mbeleni yawe mazuri kuliko yale niliyokulia.

DOWNLOAD MORE RESOURCES LIKE THIS ON ECOLEBOOKS.COM

Ecolebooks.com

Nilipojiunga na shule ya upili sikuwa na marafiki wengi. Nilianza vyema lakini nilipoingia kidato cha pili maisha yangu yalichukua mkondo mwingine. Sikushiriki michezo yoyote au chama chochote cha wanafunzi. Nilikuwepo tu! Hali hii ilinileteа upweke mkuu nami nikatafuta jinsi ya kulijaza ombwe hilo.

Nakumbuka likizo ya muhula wa tatu vyema. Nilialikwa karamuni na rafiki yangu mmoja aliyeishi karibu na kwetu. Karamuni, wengi walionekana kufahamiana na walipiga gumzo kwa uchangamfu, vicheko vilihinikiza katika mazungumzo yao. Mimi nilibaki na upweke wangu.

DOWNLOAD MORE RESOURCES LIKE THIS ON ECOLEBOOKS.COM

Ecolebooks.com

Baada ya vyakula na vinywaji kuisha. Muziki uliwekwa na vijana wakaanza kukatika. Mabatini wengi walinengua viuno nusura wakatike nyonga. Mvuli mmoja alinijia na kujitambulisha kwa jina Tido. Alikuwa na maneno mengi kama chiriku. Alikuwa akitafuna mirungi na mara kwa mara alikuwa akitia mdomoni vidonge fulani na kuvitafuna. Alinieleza kuwa vidonge hivyo vilimpa uchangamfu wa ajabu.

"Je, ungetaka kuvijaribu?" aliniuliza. Kwanza nilidinda lakini alinisihi na nikakubali. Alinipa vidonge viwili na chingamu. Nilifungua chingamu na kuanza kuitafuna. Nikakiweka kidonge cha kwanza mdomoni nikakitafuna vilevile. Hakikuwa la ladha chungu kama nilivyotarajia. Nikatia kidonge cha pili mdomoni nacho pia nikakitafuna.

Muda wa nusu saa ulipita nami nikaanza kuhoji ikiwa vidonge vile vilikuwa na athari yoyote. Fikira zile ni kama zilichochea vidonge hivyokuanza kazi. Nilihisi kichwa changu kikiwa chepesi. Mwanga wa taa ukaongezeka na utamu wamuziki ukakolea. Mimi huyoo! Nikaanza kucheza ngoma. Vijana wakashangilia. Nilipenda nilivyohisi. Nilitamani nijihisi hivyo milele.

Uraibu wa dawa za kulevya ulianzia hapo. Nilivuta bangi, nikatumia kokeni na ketamine. Sikufikiria nilikuwa katika hatari yoyote. Masomoni nilianza hushika mkia na kucheckwa na wanafunzi wengine. Nilijitafutia nafuu ya muda katika dawa za kulevya.

Jumapili moja nilialikwa na rafiki yuleyule kwao. Wazazi wake walikuwa wamesafiri naye akaachwa nyuma ili ailinde nyumba yao. Ilikuwa asubuhi na tulikuwa na siku nzima ya kujitawala kwani wazazi wake wangerudi jioni. **Waama paka akiondoka panya hutawala**. Tulikuwa na mihadarati ya aina aina. Si heroini, si kokeni, si bangi, si pombe; tulitaka kuijaribu yote. Tulichanganya yote.

Sikumbuki yote yaliyotokea. Nakumbuka tu nilitapika na baadaye kupoteza fahamu. Nilipopata fahamu nilijipata kitandani ndani ya chumba chenye kuta nyeupe. Wazazi wangu na mdogo wangu walikuwa wamesimama kando ya kitanda hicho na nyuso zao zilionyesha fazaa kuu. Ilikuwa wazi kuwa nilikuwa nimewasiliti upeo wa kusaliti. Machozi yalinilengalenga. Nilitamani ardhi ipasuke inimeze mzimamzima niondokane na aibu iliyonikabili.

**41.** Kulingana na aya ya kwanza
- A. msimulizi alikuwa katika ndoto.
- B. msimulizi hakutarajia yaliyomfika.
- C. msimulizi alikuwa na wakumsaidia.
- D. msimulizi aliyaona matumaini ya baadaye.

**42.** Aila ya mwandishi ilikuwa ya
- A. wakwasi.
- B. wachochole.
- C. walalahai
- D. mayatima.

**43.** Aya ya tatu imeonyesha kwamba,
- A. kushiriki michezo na vyama hupunguza vishawishi vya kuingilia maovu.
- B. kushiriki michezo na vyama hupunguza vishawishi vya huongeza upweke maishani.
- C. Wwote wanaoishi upweke huingilia mienendo isiyofaa.
- D. msimulizi alipenda michezo na vyama vya wanafunzi shuleni.

**44.** Wengi waliofika karamuni, A. walijuana na msimulizi. B. walitumia mihadarati.
- C. hawakuwa wamealikwa.
- D. walionyesha nyuso za furaha.

**45.** Msimulizi anaweza kutajwa kuwa, A. bendera inayofuata upepo.
- B. sikio la kufa lisilosikia dawa.
- C. nazi mbovu inayoharibu nzima.

DOWNLOAD MORE RESOURCES LIKE THIS ON ECOLEBOOKS.COM

Ecolebooks.com

D. mvumilivu alaye mbivu.

**46.** Vidonge alivyopewa mwandishi,
A. vilikuwa na ladha chungu.
B. havikuwa na athari mwilini.
C. vilimfanya kushangiliwa na wengine.
D. vilimsababishia ulevi.

**47.** Madhara makuu ya dawa hizi yalikuwa,
A. kufurahia namna alivyohisi.
B. kuzorotesha masomo.
C. kucheza densi kwa ukakamavu.
D. kuchekwa na wengine darasani.

**48.** Nikapoteza fahamu maana yake ni kuwa, Mwandishi,
A. alirukwa na akili.  B. aliangamia.
C. alizirai  D. alianza vituko.

**49.** Si kweli kusema kuwa,
A. mwandishi na mwenzake walijipata hospitalini.
B. mwandishi aliaibika kutokkana na hali yake.
C. kitendo cha mwandishi kiliwahuzunisha jamaa zake.
D. tabia ya mwandishi ilimlete majuto.

**50.** Machozi yaliyomlengalenga msimulizi yalisababishwa na
A. woga.  B. ulevi.
C. hasira.  D. aibu



DOWNLOAD MORE RESOURCES LIKE THIS ON ECOLEBOOKS.COM